



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
CHUO KIKUU CHA DODOMA



KITENGO CHA MAWASILIANO NA MASOKO

TAARIFA KWA UMMA

25 Februari, 2025

**YAH: UFAFANUZI KUHUSU TAARIFA ZILIZOSAMBAA MTANDAONI JUU
TUHUMA ZA WANAFUNZI "400" WANAODAIWA KUONDOLEWA MASOMONI**

Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Tunatoa taarifa kwa Umma kuhusu taarifa zilizosambazwa mtandaoni kuhusu wanafunzi "400" kudaiwa kufutwa masomo kwa tuhuma za kudukua mfumo. Jumamosi tarehe 22 Februari 2025, Chuo kupitia Kitengo cha Mawasiliano na Masoko, tulitoa tena taarifa kama hii, kufafanua suala hili, na tumeona ni vema kuirudia taarifa hiyo kwa faida ya wananchi ambao taarifa ya awali haikuwafikia.

Ukweli Kuhusu Wanafunzi Waliositishwa Masomo:

Katika utaratibu wa kawaida wa kukagua mifumo yake kupitia wataalamu wa Usalama wa Mifumo, Chuo Kikuu cha Dodoma kilibaini mfumo wa Kutunza Taarifa za Wanafunzi (SRMS2) umedukuliwa na hivyo kupelekea kuundwa timu ya wataalamu wa ndani wa Mifumo ya Komputa kufanya Uchunguzi. Katika uchunguzi wa awali uliofanyika, Jumla ya wanafunzi 170 walituhumiwa kuchezea Mfumo wa matokeo (SRMS2).

Kutokana na matokeo hayo, Serikali iliunda Kikosi Kazi kilichohusisha wataalamu wa Mifumo ya Kompyuta kutoka vyombo mbalimbali vya usalama, kuchunguza tuhuma hizo na kuwasilisha ripoti yao Chuo Kikuu cha Dodoma. Baada ya Chuo kupokea ripoti hiyo hatua za ndani zilianza kuchukuliwa kwa mujibu wa Kanuni za Wanafunzi wa Shahada za Awali ya mwaka 2019 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022. Hatua hiyo ilihusisha kuwapa wito watuhumiwa wote 170 kuja kusikilizwa kabla ya kutoa maamuzi kwa mujibu wa kanuni zilizopo.

Jumla ya wanafunzi 148 walisikilizwa, wanafunzi 32 hawakufika kusikilizwa. Kati ya wanafunzi (138) waliosikilizwa, wanafunzi (121) walipatikana na hatia ya kuhusika kuchezea matokeo ya mitihani; na Seneti ya Chuo iliamua kuwa waondolewe masomoni (Discontinue) kwa kukiuka kanuni. Kesi za wanafunzi (15) zinaendelea na uchunguzi zaidi, na wanafunzi wawili hawakukutwa na hatia.

Kwa mujibu wa taratibu za Chuo Kikuu cha Dodoma, mwanafunzi ambaye hajaridhika na maamuzi ya Seneti, anapewa nafasi ya kukata rufaa. Hivyo wanafunzi



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
CHUO KIKUU CHA DODOMA



ambao Hawajaridhika na maamuzi hayo, taratibu za kukata rufaa ziko ziko wazi, kupitia mifumo iliyowekwa na Chuo na inavyofahamika na wanafunzi wote.

Dirisha la rufaa hufunguliwa wiki mbili baada ya matokeo ya mitihani kutoka na kufungwa baada ya wiki mbili. Mwanafunzi ambaye yupo nje ya muda, anaruhusiwa wakati wowote kuomba kukata rufaa nje ya muda. Na kwa wale (32) ambao waliitwa na hawakufika kusikilizwa, bado wana nafasi wakati wowote kufika kusikilizwa kama kanuni zinavyoelekeza.

Chuo kitaendelea kusimamia Taratibu, Kanuni na Sheria za kimitihani ili kulinda ubora wa taaluma na hadhi ya chuo, pasipo kumuonea mtu yoyote.

Taarifa hii imetolewa na:

Rose Mdami

Mkurugenzi wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko